

## NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

Ridván 2025

Kwa Wabahai wote wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa sana,

Tukiwa tumebakiwa na mwaka mmoja tu kabla ya awamu ya kwanza ya Mpango wa Miaka Tisa kumalizika, tuna shauku ya kutoa taarifa kuhusu maendeleo yake—jinsi, kupitia mifano ing'aayo ya jitihada adilifu, muono uliotolewa na Imani unaijaza mioyo zaidi na zaidi matumaini.

Mchakato wa ukuaji unaendelea kuimarika. Mafanikio mapya ya kuvutia yametokea katika maeneo mbalimbali, ambako maendeleo makubwa hayakuwahi kushuhudiwa hapo awali, kwa kuwa mbegu ya Imani imetoa vichipukizi vipya vya kijani na uwezo wa kufanya kazi na roho nyingi kwa wakati mmoja umeanza kuibuka. Maendeleo haya mara nyingi yamewezeshwa na watangulizi waliojitoa ambao, mioyo ikiwaka kwa upendo wa Bwana wao, wameharakia kwenda kutangaza ndani na nje kwa idadi ivutiayo. Katika klasta ambako programu ya ukuaji tayari ilikwishaanza, umakinifu mpya umetolewa katika kutumia, kwa ubunifu na ustadi, ile mikakati na hatua za utekelezaji zitambulikazo ambazo zitawawezesha marafiki kuvuka hatua ya pili na ya tatu. Na katika klasta zenye nguvu iliyothibitishwa, dalili za nguvu za Imani za ujengaji jamii zinazidi kuwa wazi, kwa kuwa mtindo changamfu na ubadilishao wa maisha ya Kibah'ái unakumbatiwa na kundi liongezekalo la roho zilizoamshwa.

Wakati huo huo, ushirikiano na jamii mashinani umepiga hatua kubwa. Jitihada zenye mwelekeo wa kijamii za shughuli za kijamii zinazolenga juu ya elimu zimeongezeka kwa kasi sana, lakini jitihada zingine pia zimeendelea, katika maeneo kama kilimo, afya, mazingira, uwezeshaji wa wanawake na sanaa. Maendeleo ya aina hii yanaonekana wazi kabisa katika klasta zenye nguvu zaidi, ambapo vijiji vingi au ujirani—hata mtaa mmoja au jengo lenye idadi kubwa ya watu—ni makazi ya watu yanayopitia uinujaji unaotokana na kutafsiri kanuni za Imani kuwa uhalisia dhahiri. Katika baadhi ya maeneo, viongozi wa kiraia na watu wenye jukumu la elimu ya watoto au maendeleo ya kijamii katika ngazi ya mahali siyo tu wanawageukia Wabahá'í kwa ajili ya mitazamo, bali wanataka kushirikiana katika kutafuta suluhu za kivitendo. Zaidi ya hayo, tunafurahi kuona kwamba katika ngazi za kitaifa na kimataifa, mbinu ya Kibahá'í kwa baadhi ya mijadala muhimu inavutia fikra na haiba inayoongezeka.

Mpango wa Miaka Tisa hutegemea juu ya mchakato mkubwa wa kiulimwengu wa ujifunzaji ambao ni wenye ufanisi katika nyanda za juu za Bolivia kama ilivyo katika vitongoji vya Sydney. Mchakato huu wa ujifunzaji umeibua mikakati na hatua zinazoweza kubadilika kulingana na kila mazingira. Ni wa kimpangilio; ni wa kiasili; ukumbatiao vyote. Unaunda miunganiko, ukichanua kuwa uhusiano wenye nguvu, miongoni mwa familia, miongoni mwa majirani, miongoni mwa vijana na miongoni mwa wote walio tayari kuwa manguli katika shughuli hii tukufu. Unainua jumuiya zinazojawa na uwezo. Unawezesha utimizwaji wa matamania ya hali ya juu wanayoepana watu ambao walikuwa wametengana kwa sababu ya

kijiografia, lugha, utamaduni au malezi lakini sasa wamesikia na kuitikia mwito wa ulimwengu wa Bahá'u'lláh “kujitahidi bila kukoma kwa ajili ya uboreshaji wa maisha ya mmoja kwa mwingine.” Na unategemea kabisa juu ya nguvu iimarishayo ya Neno la Mungu—ile “nguvu iunganishayo”, “mwendeshaji wa roho na muunganishaji na mrekebishaji katika ulimwengu wa wanadamu”—na juu ya shughuli endelevu unaozivuvia.

Dhidi ya utusitusi wa anga yenye dhoruba, jinsi gani unavyong'aa mwanga unaotokana na juhudi zenu za kujitua! Hata wakati dhoruba inapochaga ulimwenguni, mahali pa usalama patakapowahifadhi wanadamu panajengwa katika nchi, kanda na klasta. Lakini kuna mengi ya kufanya. Kila jumuiya ya kitaifa ina matarajio yake kwa ajili ya maendeleo yanayopaswa kufikiwa katika awamu hii ya mwanzo ya Mpango. Muda unakwenda. Marafiki wapendwa, na watangazaji wa mafundisho matakatifu, na mashujaa wa Uzuri Uliobarikiwa—juhudi zenu zinahitajika sasa. Kila maendeleo yaliyofikiwa katika miezi inayopita upesi kabla ya Ridván ijayo yataiandaa vyema jumuiya ya Jina Kuu Kabisa kwa kile itakachopaswa kukitimiza katika awamu ya pili ya Mpango. Acha muweze kujaaliwa mafanikio. Kwa hilli tunamsihi Bwana mwenye enzi; kwa hili tunaomba sana msaada Wake usioshindwa; kwa hili tunamsihi Yeye awatume malaika Wake awapendao mno kumsaidia kila mmoja wenu.

Imesainiwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu